
Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Mauaji ya Polisi: Hulka ya Kibepari ya Ukatili na Kutokujali

**HABARI NA MAONI**
Ziara ya Usaliti

**MATOLEO**
Ni Dhambi Kubwa Kwa Ndege za Mayahudi Kuvuka Anga ya Tawala, Kuipiga Mabomu Iran na Kurudi Salama Bila Kutunguliwa na Tawala hizi Hata kwa Risasi Moja!

**JIBU LA SWALI**
Mashambulizi ya Droni na Yanayojiri katika Vita nchini Sudan



Afisi ya Habari Kenya

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

﴿ وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ كَمَا ٱسۡتَخۡلَفَ
ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمۡ دِينَهُمُ ٱلَّذِي ٱرۡتَضَىٰ لَهُمۡ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعۡدِ خَوۡفِهِمۡ أَمۡنٗاۚ
يَعۡبُدُونَنِي لَا يُشۡرِكُونَ بِي شَيۡـٔٗاۚ وَمَن كَفَرَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ ﴾

KUMB: 10/1446 Jumanne,28 Dhul Hijjah 1446 H 24/06/2025 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Mauaji ya Polisi: Hulka ya Kibepari ya Ukatili na Kutokujali

Maafisa watatu wa polisi nchini Kenya wameshtakiwa kwa mauaji ya mwanablogu mwenye umri wa miaka 31 aliyefariki akiwa mikononi mwa polisi mapema mwezi huu. Kifo cha Albert Ojwang kimezua hasira nchini Kenya huku maandamano yakifanyika kudai haki.

Sisi katika Hizb ut Tahrir Kenya, tungependa kuangazia yafuatayo

Chini ya tawala za Kisekula za Kiliberali kama vile Kenya maofisaa wa usalama ni muendelezo wa uundaji wa enzi ya ukoloni ambapo Waingereza walitumia kudhibiti idadi ya watu na kukomesha upinzani. Katika miaka ya 1950, Wakenya walipoanza kudai haki yao ya kujitawala, polisi na vyombo vingine vya usalama vilivyosimamiwa na Uingereza vilikusanya makumi ya maelfu ya Wakenya na kuwanyonga zaidi ya elfu moja. Inavyoonekana, jeshi la polisi linawaona raia wa kawaida kama tishio linalowezekana kwa utawala unaotawala njia ambayo ilianzishwa hapo awali ili kutekeleza utawala wa kikoloni-sio kulinda raia.

Kiaidiolojia, tawala za Kisekular za kiliberali huona manufaa na maslahi kuwa kipimo kikuu kipaswacho kutukuzwa zaidi hata kuliko maisha ya binadamu na mali, Kwa vipimo hivi ndio hufanya ufisadi, kutokujali na kutekwa mamlaka ya dola na genge la watu fulani ada ya kisiasa. Kwa kuzingatia hili, mauaji ya vyombo vya dola bila kuadhibiwa ndiyo njia pekee ya kuzuia sauti yoyote ya upinzani na juhudi za kufichua ufisadi mkubwa. Ni muhimu kubaini kwamba ukatili na utesaji unaofanywa na vyombo vya dola ni mtindo na tatizo la kiulimwengu wala haliko tuu kwa Kenya.

Tunasisitiza kwamba maisha ya binadamu au tuseme maisha yote ni matakatifu na hustahili kulindwa kabisa na serikali bila woga au upendeleo. Katika Uislamu, ulinzi wa maisha ya mwanadamu ni muhimu na unachukuliwa kuwa amana kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Uislamu unasisitiza utakatifu wa maisha, hivyo umeharamisha kuuwa huku ukitaka ulinzi wa maisha na heshima kwa wanadamu wote.

Tunasisitiza kwamba ni chini ya Khilafah Raashida tu (Ukhalifa ulioongoka) ambao utasimamishwa hivii karibuni juu ya mfumo wa wa Utume, jeshi la polisi litakuwa na jukumu la kudumisha utulivu wa umma, kutekeleza sheria, na kuchunguza uhalifu. Mateso ni marufuku kabisa na afisa polisi yeyote atakayepatikana na hatia ya kutekeleza unyanyasaji wa kimwili au mateso dhidi ya raia yeyote, Mwislamu au asiye Muislamu, atawajibishwa. Kwa hivyo, vikosi vya polisi vitajitolea kikamilifu kudumisha sheria na utulivu na kulinda maisha na mali za raia.


**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo Vya Habari Hizb ut Tahrir**

**Kenya**

# HABARI NA MAONI
# Ziara ya Usaliti

**Habari:**

Trump aikumbatia Pakistan: ‘mapenzi ya mbinu’ au ‘duara la ndani’ jipya?

Trump amkaribisha mkuu wa jeshi la Pakistan Asim Munir kwa chakula cha mchana cha White House ambapo haijawahi kushuhudiwa, huku Marekani na Pakistan zikirekebisha mafungano. (https://www.aljazeera.com/)

**Maoni:**

Katika wakati ambapo ulimwengu wa Kiislamu unavuja damu—kuanzia Gaza hadi Kashmir, hadi barabara za Tehran—ziara ya Jenerali Asim Munir kwa Rais wa Marekani Donald Trump si tu kwamba ni uziwi bali ni usaliti wa kiasi kikubwa. Mkutano huo, uliofanyika katika Ikulu ya White House na uliandaliwa na Trump kama ishara ya kushukuru dori ya Munir katika kutuliza hali iliyokaribia vita na India, inasifiwa na sehemu za utawala wa Pakistan kama hatua ya kimkakati ya kidiplomasia.

Kwa kweli, inaashiria sura nyingine katika urithi wa kudhalilisha wa kipote cha jeshi la Pakistan wanaosujudu mbele ya dola za Magharibi-hata kama dola hizo hizo ndizo zinazoupa silaha na kuulinda utawala wa Kizayuni katika wimbi la hivi karibuni la uvamizi wa kikatili katika Mashariki ya Kati.

Trump kumkaribisha Munir kunakuja kufuatia mashambulizi ya 'Israel' yanayoungwa mkono na Marekani ndani ya Iran, ambayo yamesababisha vifo vya mamia. Badala ya kupinga ushiriki wa Marekani katika umwagaji damu huu, Munir alinyoosha mkono kwa Trump yuleyule ambaye anafadhili na kulipa silaha umbile la Kizayuni, aliidhinisha mashambulizi ya droni katika ardhi za Waislamu, na wakati mmoja aliita Pakistan taifa la "uongo na udanganyifu." Kuwepo kwa jenerali huyo jijini Washington kunaonyesha ni kwa kiwango gani uongozi wa Pakistan umekuwa mshiriki katika mfumo wa kimataifa wa utawala wa wakoloni.

Ziara hii inaakisi miongo kadhaa ya sera ambapo viongozi wa kijeshi wa Pakistan wametanguliza kipaumbele kudumisha upendeleo kwa Washington juu ya kusimama na Umma. Trump mwenyewe aliweka wazi kwamba utawala wake unaithamini Pakistan kimsingi kwa uimarishaji wake wa kimkakati dhidi ya Iran na kwa kusaidia kudhibiti mzozo na India - maslahi ambayo yanatumikia utawala wa Marekani, sio Umma wa Kiislamu.

Kinachofanya usaliti huu kuwa mchungu zaidi ni kukatika fungamano kati ya kujitolea na mapenzi ya kina kwa Uislamu miongoni mwa watu wa Pakistan na matendo ya uongozi wake. Kuna usaliti wa waziwazi na kupuuza waziwazi wajibu wa kujisalimisha kwa amri za Mwenyezi Mungu, kuwachukulia maadui wa Ummah kama maadui, kutetea ardhi za Waislamu, na kulipizia kisasi mashahidi wao. Wajibu huo, hapa, umeachwa bila aibu.

Kwa Waislamu wa Pakistan na kwa upanuzi wao ndani ya jamii yetu: tunawakumbusha kwamba uongozi wa kweli haupigi magoti mbele ya maadui wa Uislamu, wala hauketi kimya huku Palestina na Kashmir zikiungua, na sasa Iran inavuja damu. Njia ya kusonga mbele iko katika kujitoa kamilifu kisiasa na kifikra kutoka kwa maagizo ya Amerika. Ni kwa kusimamisha tena Khilafah kwa njia ya Utume pekee ndipo nguvu za kijeshi za Pakistan zinaweza kutumika kukomboa ardhi zinazokaliwa kwa mabavu, kulinda matukufu, na kuregesha uadilifu kwa Umma. Hadi wakati huo, kila makubaliano na mhalifu wa kivita kama Trump yatabaki kuwa ukumbusho mchungu wa jinsi uongozi wa Pakistan umepotoka kutoka kwa wajibu wake wa Kiislamu.

**[يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ لاَ تَتَّخِذُواْ الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى أَوْلِيَاء بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاء بَعْضٍ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُ مِنْهُمْ إِنَّ اللّهَ لاَ يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ]**

“Enyi mlio amini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao. Hakika Mwenyezi Mungu hawaongoi watu wenye kudhulumu.” [5:51]


**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**Haitham Ibn Thbait**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Amerika**

# Ni Dhambi Kubwa Kwa Ndege za Mayahudi Kuvuka Anga ya Tawala, Kuipiga Mabomu Iran na Kurudi Salama Bila Kutunguliwa na Tawala hizi Hata kwa Risasi Moja!

Trump alisema katika chapisho kwenye jukwaa la Kijamii la ‘Truth’: ["Iran na Israel wanapaswa kufanya makubaliano, na watafanya makubaliano, kama vile nilivyozifanya India na Pakistan kufanya." Aliendelea: "Vivyo hivyo, tutakuwa na AMANI, hivi karibuni, kati ya Israel na Iran! Miito mingi na mikutano inafanyika hivi sasa."(Sky News,15/6/2025). Mnamo Jumapili, msemaji wa jeshi la umbile la Kiyahudi alisema kupitia jukwaa la X kwamba "Israel ilitoa onyo kwa Wairan wanaoishi karibu na vinu vya nyuklia nchini Iran kuhama makaazi yao." Wakati huo huo, msemaji wa jeshi la 'Israel' alisema kuwa jeshi lilishambulia kituo cha nyuklia katika mji wa Isfahan, katikati mwa Iran. Tangu alfajiri ya Jumapili, Iran ilianza kurusha raundi mpya za makombora kwenye shabaha ndani ya 'Israel', na kusababisha vifo na makumi ya majeruhi, na kusababisha uharibifu mkubwa kwa nyumba na majengo. Kwa kujibu, Tehran imekuwa chini ya mashambulizi ya 'Israeli'. (Al Jazeera,15/6/2025).

Umbile la Kiyahudi lilitangaza mnamo Jumamosi, 14/6/2025, kwamba wanasayansi 9 na wataalamu katika mpango wa nyuklia wa Iran waliuawa wakati wa uvamizi wake nchini, na hivyo kuongeza idadi ya vifo iliyotangazwa hapo awali, nao ni: Ali Bakhoy Karimi, Mansour Askari, na Saeed Borji, ambao ni wataalamu wa mekaniki, fizikia, na vifaa vya uhandisi, mtawaliwa, katika uvamizi mnamo Ijumaa, kwa mujibu wa jeshi. Hili lilikuja katika tangazo lililothibitishwa na Shirika la Habari la Tasnim la Iran. Umbile la Kiyahudi lilikuwa limeanzisha "shambulizi ambalo halijawahi kushuhudiwa nchini Iran alfajiri ya Ijumaa, 13/6/2025, likilenga kitovu cha mpango wa nyuklia wa Iran na viongozi wakuu wa kijeshi. Huku Iran ikithibitisha kwamba ilirusha mamia ya makombora mnamo Ijumaa jioni mwanzoni mwa jibu lake kwa Israel." (CNN, 14/6/2025)
Mara tu baada ya shambulizi la Kiyahudi, Rais wa Marekani Donald Trump alitangaza mnamo Ijumaa, 13/6/2025: [“Shambulizi la Israel dhidi ya Iran limekuwa bora kabisa,” akiitaka ikamilishe makubaliano kuhusu mpango wake wa nyuklia. Akijibu swali kutoka kwa ABC: "Je, kuna dori ya Marekani katika shambulizi la Iran?" alisema, “Sitaki kujibu hilo.” Alisema kwenye jukwaa la Kijamii la ‘Truth’, "Iran lazima ifanye mapatano, kabla haijapoteza kila kitu, na kuokoa kile ambacho hapo awali kilijulikana kama Himaya ya Iran." Aliongeza kuwa aliionya Tehran kwamba "Marekani inatengeneza zana bora zaidi za kijeshi zenye hatari zaidi popote duniani ... Israel inazo nyingi, na nyingi zaidi zinakuja - na wanajua jinsi ya kuzitumia." Katika taarifa mithili ya hizo, Trump alisema: "Leo ni siku ya 61. Niliwaambia la kufanya, lakini hawakuweza kufika huko. Sasa wamefika, labda, ni nafasi ya pili!" (Al Jazeera, 13/6/2025)]
Kwa kutafakari matukio haya, yafuatayo yanadhihirika:
**1-** Ni wazi kutokana na matukio haya kwamba Mayahudi hawakuishambulia Iran isipokuwa kwa amri ya Marekani ya Trump, kwani kauli zake zinaeleza haya kwa uwazi. Hili ni hakika na linatarajiwa, kwa kuwa Mayahudi hawana uwezo wao wenyewe, wala hawana uwezo wa kupigana. Mwenyezi Mungu Mtukufu, Aliyetukuka, ni Mkweli zaidi:

**[لَنْ يَضُرُّوكُمْ إِلَّا أَذًى وَإِنْ يُقَاتِلُوكُمْ يُوَلُّوكُمُ الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا يُنْصَرُونَ * ضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ أَيْنَ مَا ثُقِفُوا إِلَّا بِحَبْلٍ مِنَ اللهِ وَحَبْلٍ مِنَ النَّاسِ وَبَاءُوا بِغَضَبٍ مِنَ اللهِ وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الْمَسْكَنَةُ]**

“Maadui hawatakudhuruni ila ni maudhi tu. Na wakipigana nanyi watakupeni mgongo, na tena hawatanusuriwa. * Wamepigwa na udhalili popote wanapo kutikana, isipo kuwa wakishika kamba ya Mwenyezi Mungu na kamba ya watu. Na wakastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na wamepigwa na unyonge.” [Aal-i-Imran: 111-2]. Hivyo, tangu zama zao za mwanzo, wameikata kamba ya Mwenyezi Mungu baada ya zama za Mitume wao. Na ni vivyo hivyo katika zama za kisasa, kama vile Uingereza iliwatabanni tangu Vita vya Kwanza vya Dunia, kisha wakahamia kukumbatia Amerika baada ya Vita vya Pili vya Dunia. Vita vyao vyote vinazungumza juu ya hilo, kwa kuwa wako kwenye kamba ya watu…Usaidizi wa Trump kwao katika shambulizi lao dhidi ya Iran uko wazi kutokana na kauli za Trump hapo juu kwa yeyote aliye na moyo au anayesikiliza kwa makini.
**2-** Kisha lililo kubwa zaidi kuliko hili na la maafa na machungu zaidi ni kwamba ndege za Mayahudi zilivuka anga za tawala zinazotawala katika nchi za Kiislamu zinazozunguka umbile la Kiyahudi, ambazo ziliharibu na kuua huku zikiwa Iran na kisha zikaregea katika ardhi inayokaliwa kwa mabavu kwa usalama na amani. Hakuna hata risasi moja iliyorushwa kwa ndege hizi na watawala waliowazunguka huko Ash-Sham, Iraq, Misri, Uturuki na kutoka kila mahali… Hivyo, wanavuka mipaka na kushambulia wakiwa salama, wakienda na kurudi, na watawala katika nchi za Kiislamu wakitazama yale yaliyokuwa yakitendeka bila kuchukua hatua. Walisahau au kujifanya kusahau matokeo ya uhalifu wa kimya chao.

**[سَيُصِيبُ الَّذِينَ أَجْرَمُوا صَغَارٌ عِنْدَ اللهِ وَعَذَابٌ شَدِيدٌ بِمَا كَانُوا يَمْكُرُونَ]**
“Itawafikia hao walio kosa udhalili na adhabu kali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu ya vitimbi walivyo kuwa wakivifanya.” [Al-An’am: 124]. Ni dhambi kubwa kwamba ndege za Kiyahudi huvuka anga ya watawala vibaraka, kutekeleza mashambulizi yao na kurudi bila ya kutunguliwa na yeyote kati ya watawala hao.

***Endelea... UK 5***

**3-** Kila mwenye akili timamu anatambua kuwa njia bora ya kujilinda dhidi ya Mayahudi ni mashambulizi. Mayahudi wamekuwa wakitishia Iran kwa muda mrefu, haswa katika siku za hivi karibuni. Trump hata alidokeza na hata kutangaza kwamba Mayahudi watashambulia vituo vya nyuklia vya Iran. Hata hivyo, Iran haikuanzisha jibu la mashambulizi dhidi ya Mayahudi, katika kuilinda Iran, na kuepusha vitisho hivi kutoka kwa Marekani na Mayahudi. Hii inashangaza kwa kweli!! Iran ilikaa kimya hadi mitambo yake iliposhambuliwa na wanasayansi wake kuuawa, na ndipo ikaanza kujibu. Licha ya mashambulizi yote mfululizo, Trump anaendelea kutangaza, "Vivyo hivyo, tutakuwa na AMANI, hivi karibuni, kati ya Israel na Iran! Miito mingi na mikutano inafanyika sasa." (Sky News, 15/6/2025)! Tunatahadharisha dhidi ya vita hivi kuleta amani na umbile la Kiyahudi, bali, kama Mwenyezi Mungu alivyosema:

**[فَإِمَّا تَثْقَفَنَّهُمْ فِي الْحَرْبِ فَشَرِّدْ بِهِمْ مَنْ خَلْفَهُمْ]**

“Basi ukiwakuta vitani wakimbize walio nyuma yao ili wapate kukumbuka.” [Al-Anfal:57].

**4-** Lakini kinachovunja moyo kweli ni watawala Ruwaibidha (wajinga wasio na maana) katika nchi za Waislamu, hususan zile zinazolizunguka umbile la Kiyahudi linaloikalia kimabavu Palestina. Wanawazunguka, basi iweje wasione ndege za Kiyahudi zikipita juu ya vichwa vyao, zikipiga mabomu nchi za Kiislamu na kurudi salama bila hata risasi moja kufyatuliwa?! Badala yake, wao kana kwamba ni watu wasioegemea upande wowote wanaotazama yanayoendelea, kana kwamba wako katika nchi fulani ya mbali, si katika ardhi za Waislamu! Watawala hawa wako katika hali ya kuangamia na hilo halishangazi, kwani wako kwenye mvuto na wito wa nchi za kikoloni za makafiri hususan Amerika.

Wanasema wanachosema na kufanya wanachotaka. Wanahalalisha kutochukua hatua na kutukuza mipaka, na wakasahau au wanajifanya kusahau kuwa ardhi za Waislamu ni moja, sawa iwe ziko katika sehemu ya mbali zaidi ya dunia au iliyo karibu zaidi! Na kwamba amani ya Waumini ni moja, na vita vyao ni vimoja. Sio sawa zigawanyike kwa madhehebu yao ya Kiislamu, maadamu wao ni Waislamu, kwani wao ni Ummah mmoja:

**[إِنَّ هَذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاعْبُدُونِ]**

“Kwa hakika huu umma wenu ni umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi. Kwa hivyo niabuduni Mimi.” [Al-Anbya: 92].

Iweje ndege za adui ziruke juu ya anga ya watawala katika nchi za Waislamu na kuipiga mabomu nchi nyingine ya Kiislamu huku wao wakinyamaza kimya?! Mfano zaidi wa haya ni njia ya wale wanaotazama ndege za adui zikija na kuondoka kana kwamba haziegemei upande wowote au wako karibu na Mayahudi! Aidha, ijapokuwa watawala hawa wanasikia kauli ya Trump, sio vidokezo vyake, kwamba umbile la Kiyahudi linapigana kwa kamba (msaada) ya Amerika, amri zake, na silaha zake, lakini hakuna hata mmoja wao anayesubutu angalau kukata mahusiano na Amerika.

**[أَلَا سَاءَ مَا يَحْكُمُونَ]**

“Tazama uovu wa wanavyohukumu!” [An-Nahl: 59]

**5-** Pamoja na hayo yote, Ruwaibidha (watawala wasio na maana) hawa watatoweka na Dola ya Kiislamu, Khilafah Rashida, itaregea kuwa dola ya kwanza duniani, ikieneza kheri ndani yake, Mwenyezi Mungu akipenda. Kupigana na Mayahudi na kuondoa uvamizi wao kutatokea, Mwenyezi Mungu akipenda. Mkweli na Mwaminifu (saw) amesema katika Musnad Ahmad kutoka kwa Hudhayfah:

**«ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ...»**

"...kisha kutakuwa na Khilafah kwa njia ya Utume." Kadhalika, Al-Bukhari amepokea kutoka kwa Abdullah ibn Umar, Mwenyezi Mungu awe radhi nao wote wawili, ambaye amesema: Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) akisema:

**«..تُقَاتِلُكُمْ الْيَهُودُ فَتُسَلَّطُونَ عَلَيْهِمْ»**

“Mayahudi watapigana nanyi. Basi mtawadhibiti juu yao” Imepokewa pia na Muslim kutoka kwa Ibn Umar, kutoka kwa Mtume (saw) ambaye amesema:

**«..لَتُقَاتِلُنَّ الْيَهُودَ فَلَتَقْتُلُنَّهُمْ»**

"Kwa yakini mtapigana na Mayahudi, na mutawaua." Kisha dunia itang'aa kwa ushindi wa Mwenyezi Mungu, Mwenye nguvu, Mwenye hekima.

**[إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرَى لِمَنْ كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ]**

“Hakika katika hayo upo ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye yupo anashuhudia.” [Qaf: 37]

Kwa kumalizia, Hizb ut Tahrir, kiongozi asiyewadanganya watu wake, inakuombeni muiunge mkono na mufanye kazi nayo kuiregesha Khilafah Rashida kwa mara nyengine tena, ili Uislamu na watu wake uheshimiwe na ukafiri na watu wake wadhalilike, na huo ndio utakuwa ushindi mkubwa.

**[وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللهِ يَنْصُرُ مَنْ يَشَاءُ وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ]**

“Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu.” [Ar-Rum: 4-5]

**H. 20 Dhu al-Hijjah 1446**

**M. : Jumatatu, 16 Juni 2025Hizb-ut-Tahrir**

# Mashambulizi ya Droni na Yanayojiri katika Vita nchini Sudan

**Swali:**

Siku za hivi karibuni zimeshuhudia maendeleo ya ajabu katika vita. Droni zilishambulia Port Sudan, mji mkuu wa utawala, kwa siku sita mfululizo, na kushambulia uwanja wa ndege wa kiraia, kambi ya anga, na maghala ya mafuta, na kusababisha mgogoro wa mafuta kote nchini. Droni pia zilishambulia mji wa Kassala kwenye mpaka wa Eritrea upande wa mashariki, pamoja na miji mingine. Haya yote yalisababisha vikosi vya jeshi kuondoka kuelekea upande wa El Fasher na kuzingatia kulinda Sudan mashariki, kama BBC ilivyoripoti mnamo tarehe 10/5/2025. Je, hii ina maana kwamba shambulizi la mashariki mwa Sudan linalenga kuliondoa jeshi kutoka Darfur, na kuiacha ikiwa chini ya udhibiti wa Vikosi vya Msaada wa Haraka (RSF) pekee? Je, matukio haya ni utangulizi wa Jukwaa la Jeddah (kongamano la mazungumzo)? Au kuna malengo mengine? Shukran.

**Jibu:**

Ili kufichua madhumuni ya mashambulizi ya droni kwenye shabaha muhimu mashariki mwa Sudan, tunafafanua yafuatayo:

Kwanza: Matukio yaliyotangulia mashambulizi makali dhidi ya Sudan mashariki, hasa katika mji wa Port Sudan:

**1-** Jeshi la Sudan lilipata mafanikio makubwa kwa kuvifukuza Vikosi vya Msaada wa Haraka (RSF) kutoka miji muhimu ya kati ya Khartoum, Bahri, na Omdurman. Ushindi huu mkubwa uliongeza ari ya jeshi la Sudan, ambalo lilianza kujiandaa kuviandama Vikosi vya Msaada wa Haraka huko Darfur. Hii iliongeza ari ya jeshi kuiandama RSF ambayo inachukuliwa kuwa kawaida baada ya mafanikio haya. Mwenendo huu huwalazimu viongozi kutabanni uhalisia mpya chini ya shinikizo la raia na shinikizo kutoka kwa maafisa wa ngazi za chini wa jeshi, yaani, wale ambao hawajui mienendo ya nje:

"Mwenyekiti wa Baraza la Utawala wa Sudan, Abdel Fattah al-Burhan, alithibitisha mnamo Alhamisi azma ya jeshi kukomboa nchi kutoka kwa "mamluki na vibaraka na kuondoa Vikosi vya Msaada wa Haraka (RSF)." (Anadolu Agency, 13/3/2025). Kauli hii ililenga kutabanni uhalisia mpya, na kutokana na athari kubwa uhalisia huu mpya uliokuwa nayo kwa watu na ndani ya jeshi, sekta za jeshi zimeanza kupambana na RSF katika baadhi ya maeneo ya Darfur. Vikosi vya Jeshi vimetetea kwa ushujaa nafasi zao. Mji wa El Fasher ndio pekee kati ya miji mikuu mitano ya Darfur ambayo imesalia chini ya udhibiti wa jeshi. Jeshi la Sudan limeanza kukimbilia Darfur.

"Matukio ya hivi punde yanaashiria kusonga mbele kwa vikosi vikubwa vya jeshi na vikosi vya pamoja kutoka mji wa kaskazini wa Ad-Dabba ili kuondoa mzingiro wa El Fasher, huku vikosi vyengine vinavyoshirikiana na vikundi hivyo vikikimbilia majimbo ya Kordofan na kupata ushindi mkubwa katika njia yao ya kuelekea mji huo kutoka mhimili mwingine." (Al-Quds Al-Arabi, 19/4/2025). Mwenendo huu, ambao watu wanausukuma baada ya ushindi wa Khartoum na ulio na mvuto mkubwa ndani ya jeshi, sio mtazamo wa Marekani. Kwa hiyo, Al-Burhan alijaribu kudhibiti mwelekeo huu. (Al-Burhan alionya dhidi ya kampeni za upotoshaji zinazokuza wazo kwamba vita vinalenga makabila maalum, akisisitiza kwamba "vita vyetu ni dhidi ya mtu anayebeba silaha dhidi ya serikali, sio dhidi ya kabila lolote," akizingatia kwamba uvumi huu unalenga "kuhamasisha watu na kuwaburuza katika mauaji." Alifafanua kuwa "uasi wa kiongozi wa kikabila haimaanishi kabila zima," (RT, 29/4/2025). Ilikuwa ni kana kwamba alitaka kusitisha haraka msafara wa jeshi kuelekea Darfur, kutokana na kwamba baadhi ya makabila ya huko yanaamini kwamba jeshi liko dhidi yao, kana kwamba anaomba kucheleweshwa.

**2-** Baada ya kushindwa vibaya na RSF katika eneo la kati na kupoteza sehemu zao kuu jijini Khartoum, Bahri na Omdurman, na pia kupoteza wapiganaji wao wengi na makamanda wa uwanja, waligubikwa na kushindwa na udhaifu. Kisha wakaelekea kwenye ngome yao huko Darfur, ambayo wengi wao waliidhibiti, na wakauzingira mji wa El Fasher. Jumuiko hilo la Vikosi vya Msaada wa Haraka lilikuwa kwa mujibu wa maagizo ya Marekani kwa Sudan. Ni jambo la kawaida, kutokana na mazingira, kwamba baadhi ya RSF wangetawanyika na kukabiliwa na ugumu wa kusajili kutoka kwa makabila ya tiifu, ikizingatiwa kwamba walikuwa wakipigana vita vya kushindwa dhidi ya mpinzani mwenye nguvu, jeshi la Sudan. Hii ina maana kwamba ari ya RSF ilikuwa chini. Kwa hiyo, vikosi vya jeshi mjini El Fasher vilitosha kurudisha nyuma mashambulizi yao ya mara kwa mara, ikimaanisha kwamba mashambulizi yao dhidi ya El Fasher hayakuwa na kasi. Kwa hiyo, jitihada kubwa zilihitajika kurejesha ari kwa majeshi ya Hemedti na kuonyesha ubora na nguvu zao, na uwezo wao wa kushambilia na kutishia maeneo ya mbali ambayo yalikuwa salama kwa jeshi la Sudan, kama vile Sudan ya Mashariki.

**3-** Licha ya utiifu wa watawala wao kwa Waingereza, Imarati (UAE) imeendelea kumuunga mkono kibaraka wa Marekani na kamanda wa Rapid Support Forces (RSF), Mohamed Hamdan Dagalo (Hemedti), kwa

***Endelea... UK 7***

matumaini ya kupata ushawishi juu yake na wafuasi wake. Kitendo hiki ni sawa na kile inachokifanya nchini Libya kwa kumuunga mkono kibaraka wa Amerika, Haftar. Sudan imerudia kueleza kutoidhinishwa kwake na UAE na kuituhumu kwa kutoa msaada mkubwa wa kijeshi kwa RSF. Katika kujibu tuhma hizo, UAE ilifunga ubalozi wake nchini Sudan na haikuuhamishia mjini Port Sudan, kama nchi nyingine zilivyofanya baada ya kuzuka kwa vita jijini Khartoum mnamo Aprili 2023. Hata hivyo, Sudan iliendelea kudumisha ubalozi wake nchini UAE. Kwa kuzingatia hasira hii na kuzidi kwake, Sudan ilifungua kesi dhidi ya UAE katika Mahakama ya Kimataifa ya Haki, ikiituhumu kushiriki katika mauaji ya halaiki yaliyotekelezwa na RSF nchini Sudan. Hata hivyo, mahakama hiyo ilikataa ombi hili la Sudan:

"Mahakama mnamo siku ya Jumatatu ilisema haiwezi kuhukumu kesi dhidi ya UAE, ilikataa ombi la Sudan la hatua za dharura na kuamuru kesi hiyo kuondolewa katika orodha yake." (Reuters, 6/5/2025). Kisha Sudan ilichukua hatua nyingine kali dhidi ya UAE, kukata mahusiano ya kidiplomasia na UAE na na kuondoa ubalozi wa Sudan. Kisha, matukio yanayohusiana na UAE yaliendelea. "Jeshi la Sudan lilitangaza mnamo siku ya Jumapili kuangamizwa kwa ndege ya mizigo ya Imarati iliyokuwa imebeba vifaa vya kijeshi kwa Vikosi vya Msaada wa Haraka... Ilisema kuwa ndege hiyo ilikuwa imebeba vifaa vya kijeshi, ikiwa ni pamoja na droni za kujiua na droni za kimkakati." (Sudan Tribune, 4/5/2025).

Pili: Madhumuni ya maendeleo haya na matokeo yake:

**1-** Kutokana na kuongezeka kwa mapigano jijini Khartoum tangu 2023, Baraza la Utawala lililazimika kuhamishia mji mkuu kwa muda hadi mji wa Port Sudan, ikizingatiwa kuwa ni eneo salama zaidi. Misheni za kidiplomasia za kigeni, mashirika ya kimataifa ya kutoa misaada, na wakaazi wengi waliokimbia eneo la kati kwa ajili ya usalama walihamishiwa na wanachama wa Baraza Kuu, na kuwa wakimbizi. Eneo hili linawakilisha uhai kwa Sudan wakati wa vita – kwani liko na bandari inayoleta bidhaa kutoka nje ya nchi na uwanja wa ndege pekee wa kimataifa unaofanya kazi nchini humo, huku uwanja wa ndege wa Khartoum ukiwa bado umefungwa licha ya kuwa chini ya udhibiti wa jeshi. Kama mshipa muhimu wa uhai na makao ya serikali ya mpito, mashambulizi ya mfululizo ya droni kwa siku kadhaa yalikuja kama mshtuko mkubwa kwa umma wa Sudan na jeshi. Mashambulizi haya yanaonyesha kuwa RSF sio nguvu ambayo imevunjwa, kama wengine walivyofikiria, lakini wana uwezo mkubwa zaidi kuliko walivyoonyesha hapo awali. Pia zinaonyesha kwamba jeshi halipaswi kutawanyika katika majangwa ya Darfur, lakini linapaswa kuimarisha na kulinda huduma hizi muhimu, kama vile bandari, uwanja wa ndege na maghala ya mafuta. Zaidi ya hayo, moto mkali uliozuka katika maghala ya mafuta unapendekeza kwa jeshi kwamba huduma zake za kilojistiki, muhimu kwa vita huko Darfur, zimeharibiwa, kwa hivyo ni lazima kuchukua muda wake na kuzirekebisha kabla ya kukimbilia Darfur.

**2-** Mashambulizi hayo kwenye vituo vya Port Sudan, Uwanja wa Ndege wa Kassala, na kituo cha Wanamaji cha Flamingo yalifanywa na droni za China, kulingana na uchambuzi kutoka kwa vyanzo kadhaa, ikiwemo BBC, tarehe 10/5/2025. Droni moja inaweza kubeba kilo 40, huku nyengine inaweza kubeba kilo 200 za vilipuzi na makombora ya kuongozwa. RSF haijawahi kutumia droni kama hizo hapo awali. Droni mithili ya hizo zimeonekana kwenye Uwanja wa Ndege wa Nyala, ambao unadhibitiwa na Vikosi vya Msaada wa Haraka. Huu ndio uwanja wa ndege ule ule ambapo jeshi lilisema liliangamiza ndege ya mizigo ya Imarati.

**3-** UAE ilikuwa miongoni mwa nchi za kwanza katika eneo hilo kupata droni za China miaka iliyopita. Mnamo tarehe 2/5/2019, Habari za Ulinzi ziliripoti kwamba UAE ilitumia droni hizi kumuunga mkono Khalifa Haftar katika mashambulizi yake jijini Tripoli, Libya. Shirka la 'Times Aerospace' iliripoti kwamba UAE ilitumia droni hizi za Kichina kushambulia maeneo ya wanajihad nchini Iraq na Afghanistan mwaka 2014. Hii ina maana kwamba UAE imekuwa na silaha za aina mbalimbali nzito za droni za Kichina kwa miaka mingi, na kuna uwezekano kwamba wao wako nyuma ya mashambulizi haya mashariki mwa Sudan, ama moja kwa moja kutoka baharini au kwa kuzipatia RSF. Wamekasirishwa na kukashifu kwa serikali ya Burhan Mahakama ya Kimataifa, kukata mahusiano nao, na kuangamizwa kwa ndege yao ya mizigo.

**4-** Angazo la mashambulizi hayo lilikuwa kwenye viwanja vya ndege, bandari, na kambi ya wanamaji ya Flamingo. Moto mara nyingi ulizuka, na kuchukua masiku kuudhibiti, ikionyesha kuwa maghala ya mafuta yalikuwa yakilengwa. Waziri wa Nishati na Petroli wa Sudan, Muhieddin Mohamed Naeem, alifichua kuwa bohari tano kuu za kuhifadhi mafuta ziliteketezwa kutokana na mashambulizi ya droni katika siku ya kwanza ya kampeni (Sauti ya Sudan, 6/5/2025). Kutokana na kuendelea kulenga vituo vya nishati, waziri huyo alitoa maagizo ya kufungwa kwa bomba la kubeba mafuta ya Sudan Kusini kutokana na ulipuaji wa droni katika kituo cha kusukuma mafuta mashariki mwa Atbara (Al Jazeera Net, 11/5/2025).

**5-** Ulengaji huu ulilenga mafuta, ili kulinyima mafuta jeshi la Sudan, jambo ambalo lingezuia kuanzisha operesheni kubwa huko Darfur, haswa katika mji wa El Fasher. Hii ni pamoja na kuionyesha serikali katika nafasi dhaifu, kwani haiwezi kulinda makao yake makuu, pamoja na kupata mafuta na umeme kwa mahitaji yote ya Sudan. "Kampuni ya Umeme ya Sudan ilitangaza kwamba "kituo cha umeme cha Sudan kiliharibiwa kwa sababu ya kulengwa na droni na kukatika kwa umeme." (Anadolu Agency, 8/5/2025)

***Endelea... UK 8***

**6-** Ni wazi kutokana na hayo yote kwamba mashambulizi makubwa ya mashariki mwa Sudan hususan kwenye vituo vya kimkakati vya mji wa Port Sudan yanahusishwa na vita vya Darfur. Wanalenga kulazimisha jeshi kuondoka kushambulia El Fasher na kuelekea mashariki kutetea Port Sudan. BBC iliripoti mnamo tarehe 10/5/2025, kwamba vikosi vya jeshi vilivyokuwa vinaelekea El Fasher vililazimishwa na shambulizi la mashariki mwa Sudan kuregea na kuangazia kulinda Sudan mashariki.

**Tatu:** Hitimisho la Matukio haya

**1-** Inaelekea kwamba, baada ya mashambulizi hayo mazito, jeshi la Sudan limeanza kuhofia uwezo mpya wa Vikosi vya Msaada wa Haraka na kupoteza uwezo wa kupata mafuta yanayohitajika kuendesha magari yake katika vita walivyopanga El Fasher na Darfur kwa jumla. Hii ni pamoja na haja ya kuimarishwa kwa Sudan mashariki kwa hofu ya mawimbi zaidi ya mashambulizi, na hivyo kupunguza shinikizo la jeshi kwa Darfur na wasiwasi wake na eneo la mashariki.

**2-** Kuhusiana na RSF, vikosi vyake vitashika kasi na kuwa katika ari bora ya kufikia matokeo huko El Fasher, yote yakiwa na msaada kutoka UAE na utoaji wa droni nzito za China.

**3-** Inatarajiwa kuwa mashambulizi dhidi ya El Fasher yataongezeka na kwamba sekta za jeshi zilizokuwa zikielekea kumuunga mkono El Fasher zitarudi nyuma, na kwamba Baraza Kuu litachukua muda kurekebisha uharibifu huu mashariki mwa Sudan. Haiwezekani kwamba mazungumzo ya Jeddah yataanza tena kabla ya RSF kuchukua udhibiti wa El Fasher, au kuwa na uzito ndani yake, ambayo ni muhimu katika Darfur. Kisha Amerika itaunda usawa wa nguvu na udhibiti kati ya vikosi viwili vya Sudan (jeshi na Vikosi vya Msaada wa Haraka), ili kwamba ikiwa mazungumzo ya Jeddah yataanza tena, RSF itakuwa imetupilia mbali vazi la kushindwa na itasimama kwa ujasiri katika nguvu zao na uthabiti wa udhibiti wao na kuwa wameanzisha serikali ya kweli huko Darfur, yaani, kuunda hali zinayofaa kwa mgawanyiko kuwa tayari na kuwa uhalisia ambao lazima ukubaliwe.

**Nne**: Inatia uchungu kwamba mkoloni kafiri Marekani inaweza kusimamia vita vinavyotoa uhai nchini Sudan na kuwatumia vibaraka wake kuvitekeleza kwa uwazi, si kwa siri, na hadharani, bila kufichwa. Burhan na Hemedti wanapigana na damu ya watu wa Sudan bila sababu yoyote isipokuwa kutumikia maslahi ya Amerika, kwani inataka kurudia mgawanyiko wa Sudan kama ilivyokuwa katika kutenganisha kusini na Sudan. Sasa inafanya kila iwezalo kutenganisha Darfur na mabaki ya Sudan. Kwa hivyo, jeshi linaelekeza umakini wake katika maeneo mengine ya Sudan, na RSF inaelekeza umakini wao katika Darfur. Iwapo watu wenye ikhlasi ndani ya jeshi watajishughulisha katika kuregesha udhibiti wa Darfur, RSF itahamishia vita katika maeneo mengine nchini Sudan ili kulivuruga jeshi, hivyo basi vikosi vyake vitaondoka Darfur hadi mashariki mwa Sudan, ambapo RSF inazidisha mashambulizi yao kwa kutumia droni. Hii ni kuwezesha RSF kuchukua udhibiti kamili wa Darfur!

Kwa kumalizia, tunakuombeni kwa namna ile ile kama tulivyokuombeni katika jibu letu la awali la tarehe 19/12/2023:

Enyi watu wetu nchini Sudan ya Uislamu Mtukufu... Sudan ya Msikiti wa Dongola, msikiti wa kwanza kujengwa na Waislamu wa kwanza Sudan... Sudan ya ushindi mkubwa wa Kiislamu katika zama za Khalifa Othman, Mwenyezi Mungu amuwie radhi, ambapo alimuamuru gavana wa Misri kuleta nuru ya Uislamu Sudan, hivyo akawatuma askari wa Uislamu wakiongozwa na Abdullah Ibn Abi Al-Sarh, na kufunguliwa kwake kukatokea mwaka wa 31 H. Na kwa hivyo, Uislamu ukaenea kwa kasi, kwa upendeleo wa Mwenyezi Mungu, mpaka ukaijaza Sudan yote: kutoka kaskazini hadi kusini yake na kutoka mashariki hadi magharibi yake ... Kisha ukaendelea wakati wa zama za makhalifa wa Waislamu.

Enyi watu wetu wa Sudan, mliopigana dhidi ya Waingereza kuanzia 1896 hadi katikati ya Vita vya Kwanza vya Dunia mwaka 1916, wakati shujaa mchamungu na hodari, Ali bin Dinar, Wali (gavana) wa Darfur, alipouawa shahidi. Mwanachuoni huyo na mpiganaji huyo alisifika kwa kufanya ukarabati Miqat ya Madina na watu wa Ash-Sham, Dhu al-Hulaifah, na kujenga visima vya kunyweshea maji mahujaji, ambavyo bado vinaitwa kwa jina lake hadi leo, Abyar Ali.

Enyi watu wetu wa Sudan, tunawaomba murekebishe hali kabla ya majuto, kwa maana hakuna wakati wa kujuta. Chukueni udhibiti wa pande mbili zinazopigana na muwaunge mkono kwa uthabiti kwenye njia sahihi. Inusuruni Hizb ut Tahrir katika kusimamisha Khilafah Rashida, kwani ndani yake umo utukufu wa Uislamu na Waislamu na udhalili wa ukafiri na makafiri. Na radhi za Mwenyezi Mungu ni kubwa zaidi.

**[إِنَّ فِي ذَلِكَ لَذِكْرَى لِمَنْ كَانَ لَهُ قَلْبٌ أَوْ أَلْقَى السَّمْعَ وَهُوَ شَهِيدٌ]**

“Hakika katika hayo upo ukumbusho kwa mwenye moyo au akatega sikio naye yupo anashuhudia.” [Qaf: 37]

**23 Dhul Qi’dah 1446 H**

**21 Mei 2025 M**